JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI**

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**Kumb. Na: EB.32/160/01/244** **16 Juni, 2025**

Mkurugenzi Mtendaji,
SG Five Radio Limited,
S. L. P. 6963,
**47101 DAR ES SALAAM.**

## AMRI YA UTEKELEZAJI

*(Imetolewa kwa mujibu wa kifungu cha 48 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania, Sura ya 172 ya Sheria za Tanzania)*

1. Tarehe 11 Oktoba, 2021 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (ambayo inarejewa kama "Mamlaka"), ilitoa Leseni ya Huduma za Utangazaji kwa njia ya Redio (ambayo inarejewa hapa kama "Leseni") kwa Kampuni ya SG Five Radio Limited (ambayo inatambuliwa hapa kama ("Mleseni") kwa ajili ya utoaji wa huduma za Utangazaji kwa njia ya Redio;

2. Leseni iliyotolewa kwa Mleseni inamtaka Mleseni, wakati akitoa huduma, kufuata Sheria, Kanuni, Masharti ya Leseni, miongozo na maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Mamlaka;

3. Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2022 kikisomwa pamoja na Kanuni ya 10(1) ya Kanuni za Leseni za mwaka 2018 zinamtaka Mleseni kulipa ada za Leseni kama zilivyoainishwa katika Kanuni husika;

4. Mamlaka katika kutekeleza majukumu yake ya kiudhibiti, mara kwa mara imekua ikimkumbusha Mleseni kutimiza wajibu wake kisheria wa kulipa ada za Leseni lakini pamoja na kukumbushwa Mleseni ameshindwa kutimiza wajibu wake;

5. Kifungu cha 21 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2022 kimeainisha kuwa, Mleseni anapokuwa ameshindwa kulipa ada za Leseni kwa kujirudia, anakua ametenda kosa kubwa ambalo linaweza kupelekea kufutwa kwa Leseni ya utoaji huduma;

Mawasiliano Towers, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Fax: +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz
ISO 9001:2015 Certified

6. Kifungu cha 22(a) na (c) cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2022 kinaipa nguvu Mamlaka ya kufuta Leseni au kusitisha utoaji huduma kwa Mleseni pale ambapo Mleseni husika anapotenda kosa kubwa kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 21 cha Sheria hii; na

7. Rekodi za Mamlaka zinaonesha kuwa, wakati akiwa anatoa huduma zinazosimamiwa na Mamlaka na pamoja na kukumbushwa na Mamlaka mara kadhaa, SG Five Radio Limited imeshindwa kulipa ada za Leseni na kupelekea malimbikizo ya ada hizo kufikia kiasi cha **Shilingi za Kitanzania Milioni Kumi, Laki Moja Sabini Elfu (10,170,000/=)** kinyume na matakwa ya Kifungu cha 15(1) cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, Sura ya 306 iliyofanyiwa mapitio mwaka 2022 ikisomwa pamoja na Kanuni ya 10(1) ya Kanuni za Leseni za mwaka 2018.

**HIVYO BASI**, SG Five Radio Limited inaamriwa, kuwasilisha maelezo ya maandishi na kufika katika Ofisi za Mamlaka Kanda ya Ziwa, Mwanza tarehe **25 Juni, 2025, saa nne (4:00) asubuhi,** ili kutoa utetezi wa kwa nini hatua zaidi za kisheria na kiudhibiti zisichukuliwe dhidi ya SG Five Radio Limited kwa ukiukaji wa Sheria, Kanuni, na Masharti ya Leseni.

Iwapo SG Five Radio Limited itashindwa, itazembea, au kukataa kutekeleza amri hii, Mamlaka itaendelea kuchukua hatua zaidi za kisheria na kiudhibiti dhidi SG Five Radio Limited kwa mujibu wa Sheria.

Amri hii imetolewa tarehe **16** mwezi **Juni, 2025.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Mon Jun 16 13:59:35 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Amri hii imepokelewa na SG Five Radio Limited tarehe ....19........ **Juni, 2025.**

Jina: SAMWEL MAHELA

Sahihi: ..........................................

Cheo: MKURUGENZI

(muhuri)

SG FIVE ...
91.3 ... KIG...
... 63
DAR ES SALAAM
DATE ...

Mawasiliano Towers, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
Simu +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 Fax: +255 22 2412009-10
Barua pepe: barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, Tovuti: www.tcra.go.tz
ISO 9001:2015 Certified